MAHUBIRI N°10: UFUNUO WA WANA WA IBILISI

(*Ilihubiriwa jumapili asubuhi 23 februari 2003 pa Locodjro, Abidjan - Côte d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

Je! Mumekwisha kuona namna ya majengo makuu sana ya kidini ya Abidjan, kanisa kuu Mtakatifu-Paulo? Ni wavu ya uvuvi iliyo tupwa na Shetani. Na hiyo ni mfano ya majengo yote ya kikristo mbali mbali na ujumbe huu. Ni nyavu za Shetani. Mbali mbali na ujumbe wa unabii utokao kwa Mungu, ni nyavu za Shetani.

Hizo miaka kumi za mwisho, tunakuwa tukiona katika kila taifa, vyama kubwa kubwa vya upako chini ya utawala wa T.L Osborn, Benny Hinn, Morris Cerullo, Reinhard Bonnké, manabii na ma prezidenti wa makanisa, na ni ile nitakayo zungumzia siku hizi. Wamejaza dunia na mauti lakini ujumbe huu pia utavuma siku zote kama kengele ya mazishi ya utawala wao mbovu na haribifu. Na ikiwa shetani ambaye jina lake ni Osborn na aliye poromoshwa katika hali ya mwanadamu akisimama pale, nitamwambia hayo kwa sauti kubwa! Ndio wale Biblia inazungumzia katika Mat.24:24, 2 Tes.2:9-12 na Ufu.16:13-14. Na wachawi hao wameshikiliwa na zawadi kuu za unabii, kutambua na kunena kwa lugha…wamekwisha kupokea muhuri wa upotevu, chapa cha mnyama. Wanaweza kuona na kufahamu tu kama roho ya uovu inawaruhusu na hii ndio hali ya dunia ya kipagani na ya kidini. Watu hawaelewi namna gani hiyo "roho mtakatifu" inayo tenda, kunena kwa lugha, inayo tabiri kweli, kufanya miujiza, inayo tetea watu wasio stahili ili wakaribie meza ya Bwana, [hawaelewi] kwamba inaweza kuwa roho ya uovu. Wabatisti, kusanyiko za miungu, wapentekoste, hawawezi kukubali maneno haya. Wakatolika hawawezi kubali kwamba papa anaweza kuwa katika kosa na ni sawa kwa kila kanisa na kwa kila kiongozi wao. Sababu gani? Shetani amekwisha kuwateka nyara wote. Tayari wamekwisha kupokea chapa cha kupofushwa. Biblia inasema kwamba wao ni maskini, vipofu, wanyonge na uchi na wanajiita matajiri wasiyo na haja ya kitu. Ni shetani inayo wapa kufikiri hivi. Shetani anawaambia: *"kanisa haiokowi! Ukimwamini Yesu na hapo unajitakasa ile ndio ya muhimu "!* ulaaniwe! [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina!*]. *"ukibatizwa kwa jina la Yesu Kristo au kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu, yote ni sawa "*. ulaaniwe! Alaaniwe mtu ambaye kinywa chake kinaweza kutoa neno kama hili! [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina!*]*…" Kuna aina ya suruali kwa wanawake"*, ulaaniwe! [*Ndl: kusanyiko linasema: Amina!*]. Hata pia mwanamume hawezi kuvaa huo uvumbuzi wa Shetani. *"Roho inayotenda ndani ya makanisa za ujumbe wa jioni ni Roho Mtakatifu!"* ulaaniwe! [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina!]*. *"Mwafrika hawezi kuwa nabii mjumbe kwani yeye ni uzao wa Hamu!"*, ulaaniwe! [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina!*]. munaona? Siku moja, ni katika 2 Mambo ya Siku 35, Yosia aliye kuwa nabii na Mfalme wa Yuda akakutana na mwafrika moja kwa wakati Mungu hakuwa akisema na watu wa mataifa, na farao alimwambia: « *ondoka njiani mwangu kwani Mungu unaye muabudu alisema nami…* » lakini huyu mfalme mwema hangeweza kukubali kwamba Mungu alisema pia na mweusi ndipo akafariki pale! Munaona? Alaaniwe yeyote anaye jaribu kufahamu au kutafsiri Neno la Mungu kwa namna yake ya upekee. Unasema: *"Ufufuko tayari umepita!"* ulaaniwe! *"Mtu hapotezi wokovu basi ninaweza kufanya zambi! Sitapata tu zawabu lakini ninaokolewa! "* ulaaniwe! [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina!*]. Na kwa sababu haupaswi kupata zawabu duniani kama Mbinguni, basi yeyote atakaye kupatia zaka, sadaka wala zawadi fulani alaaniwe milele. [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina!*]. *"nimebatizwa kwa jina la William Branham"* ulaaniwe! Ni kusema nini? *"mimi ni mubatisti"*, ulaaniwe! *"mimi ni kusanyiko la miungu"*, ulaaniwe! *"mimi ni mkatolika "*, ulaaniwe! Munaona? *"Mungu abarikiwe, nimefanya mafunzo ya teolojia..."*, ulaaniwe! Munaona? Wandugu walikuja hapa na vyeti vya ukombozi vinavyo onyesha kwamba wamekombolewa toka mapepo wachafu wa aina yote, tulizichoma zote pamoja na barua za kujieleza maisha… Watu wanaendelea kutumikia na kuabudu shetani kwa jina la Yesu. Wanafikiria kwamba hao ma Yesu ndogo ndogo wa makanisa wanao wadanganya wanaweza kufanya jambo fulani kwa muchaguliwa aliye macho wazi…

Ninaona watu wakifanya maombi kwa namna hii: *"Bwana, bariki huu mkutano au chakula hiki… kwa jina la Yesu ! Amina !"*. Ikiwa Yesu ni Mungu Mwenyezi, basi ni nani walimuomba kwa jina la Yesu?... munaona? Katika hizi nyakati za mwisho, Mungu anajionyesha kama tai kubwa kama inavyo andikwa katika Ufu.12:14 na watoto wake [wanaonekana] kama tai wadogo wadogo watakao kusanyika kando ya Neno la unabii. Na kwa wakati ule, shetani anajifunua kama nyoka katika ile shairi, roho ya uchawi, na imejaza makanisa. Yeyote anaye tupilia mbali mahubiri ya Mat.25:6 atapokea tu roho ya uchawi kama roho mtakatifu. Yeyote asiye kusanya pamoja nasi anasambaza. Huu wingi wa manabii duniani kote wanamtumikia nani ijapo wametupilia Kweli? Tayari Biblia imetuambia katika 2Tes.2:9-12 na katika Mat.24:24 kwamba Mungu mwenyewe atawatuma na miujiza na alama kwa wale wasio na upendo kwa kujua Kweli ili waamini mambo haya na wapate kuhukumiwa. Tunawakuta katika Ufu.16:13-14. Munaona? Mambo haya yamefikia ukamilifu wake hizo miaka kumi za mwisho. Uongofu wote nje ya kelele ya katikati ya usiku ni makutano ya shetani kwa mateso itakayo kuja. Ni ufunuo wa wana wa ibilisi.

Munaona? Yesu Kristo alisema kwamba nabii wowote hapokelewi katika mji wake lakini wote hao ni manabii tu katika nchi zao binafsi. Nje ya nchi yao wao si kitu! Lakini ukristo inapokelewa zaidi katika nchi nyingine kuliko Israeli. Lakini hao wanapokelewa na wana kusanyiko kubwa kubwa tu katika nchi zao binafsi. Munaona? Lakini tangu tarehe 18 desemba 2005, mutaona kelele ya katikati ya usiku ikifikia kila mji duniani kama tetemeko la nchi pasipo mtu kuinyamazisha.

Na katika Ufu.16:13-14 tunaona hivyo vyura: hizo makanisa za kiprotestanti, za kiinjili na za kibranhamisti. Ninahakikisha kwamba wafalme wanao tajwa pale siyo wafalme kwa kanuni… Haya! Vyura ni katika maji chafu, maji mekundu, maji isiyo telemuka na inayonuka ijapokuwa samaki ni katika vilindi, katika maji meupe, safi na inayotelemuka.

Mungu ni upendo lakini yeye ni Mungu wa hukumu vilevile. Ni pia katika wema wake kuu ndipo aliumba jehanam. Fwateni makanisa! fwateni manabii wa uongo! Furahini katika makanisa zenu, tembeeni katika tamaa ya mioyo zenu! Nimewaonyesha Yesu ambaye mumemusulibisha upya. Lakini kwenu muliyo pendezwa na Kweli, muwe wenye hekima! Musisome hata moja ya vitabu vile, vitabu ndogo ndogo, wala barua zao visipatikane kwenu hata kidogo! Hata maandiko ya Ewald Franck. Mushike tu ujumbe wa katikati ya usiku na Biblia. Ikiwa munaamini kwamba mimi ni mtu wa Mungu, basi pokeeni hiyo kama amri. Musijichafue! Kumbukeni Ufu.14:4,5. Ni hivyo pia itamubidi Bibi Arusi wa Kristo kuonekana. Pokeeni yote niliyo waambiya ninyi kama amri. Musijaribu kucheza na nyoka kama Eva. Mujitenge mbali na uso wake. Musitwae hata moja iliyo yao kwani

inatubidi tuwe pasipo taka wala sura kukunjama. Someni na someni tena mahubiri haya, ni Roho na Uzima. Yesu aliwaambia wafwasi wake wajikinge na chachu yao. Mat.16:5-12. Vitabu vyao, kaseti za [nyimbo za] sifa, na kazalika… munaona?

Zamani, kusema: *"mimi ni mkristo"* ilikuwa haya katika jamii, haukupokelewa wakati ulipo sema hivi. Lakini sasa ni tofauti, neno "mpagani" ni kama matukano. Lakini kwa kweli, siyo wakristo wala makanisa na ni shetani aliye fanya mambo haya. Ni kama hizo *agano jipya za Gideoni* zinazo gawanywa katika makanisa, shule, hospitali, hoteli na vingine. Namna gani shetani aliyezuia kusoma Neno la Mungu anaweza je kuruhusu igawanywe popote? Siyo neno la Mungu! Musidanganyike!

Alama ingine ya udanganyifu wao, ni upako wao. Upako ulikuwa ngumu sana juu ya sanduku ya Kacou Séverin kwa namna haingeweza kuguswa kwa muda fulani. Haiwezekani kuingia katika gari ya wamoja wamoja na nilisikia kwamba baada ya nabii kutoka katika choo, upako ulibaki pale. Munaona? Lakini tuangalie sasa Yesu alikuwa namna gani, yeye wanao jidai kumtumikia. Someni Luka 8: 43 mpaka 45: *«Na mwanamke mmoja mwenye kupoteza damu tangu miaka kumi na miwili… akamkaribia nyuma yake na akagusa upindo wa nguo yake; na mara moja upotevu wake wa damu ukakoma. Na Yesu akasema: ni nani aliyenigusa? Na kwa namna wote walikana, Petro akasema, pamoja na wote waliyokuwa naye: Mwalimu, makutano wanakuzunguuka na kukusonga, na unasema: ni nani aliyenigusa?».* Munaona? Hata mwanamke, wala wafwasi, hata mtu mmoja katika makutano wanaozunguuka na kusonga Yesu upande wote hakuanguka. Iwe katika kipindi hiki, hata nafasi ingine katika Biblia. Kwa nini basi mtu ataanguka? Ni shetani aliyekuwa msingi wa hararati hii munayoona na ambayo itapita siku si nyingi. Unasema: *"Ndugu Filipo, kwa wengine ilikuwa Roho ya Mungu!"*. Ninawaambia HAPANA ndugu zangu, ni Shetani kwa upande wote. Neno la nabii. Nje ya ujumbe huu, watu wanaponenea ubatizo wa Roho Mtakatifu, mufahamu hapo, ubatizo wa mapepo. Munaona? Yesu mwenyewe alikuwa Mungu, Mtakatifu, pasipo zambi… mara watu walimugusa pasipo kuanguka basi ninyi, mumezaliwa katika zambi na ninyi ni watenda zambi, makutano wanaanguka pasipo hata kuwagusa? Mujitambue! Chagueni haya mbele ya watu kuliko jehanamu, kwani kama mimi ni nabii sasa ninasema kwamba yeyote alifanya mambo haya wala kufwata wala kushikilia mmoja ya watu hawa wenyi upako, tayari amesahihi hukumu yake mwenyewe.

Tena nendeni mukatazame michango na wizi katika makanisa za kiinjili na mutaona kwamba makanisa haya yalifanya mabaya zaidi kuliko mama yao, kanisa katolika. Mchungaji wala nabii anageuka mfanya biashara ya injili na mwenye zambi anageuka mnunuzi. Ndio maana hawawezi kusema nanyi kama ninavyo sema nanyi asubuhi ya leo. Na mwenye zambi anapoona vyombo vya nyimbo na chama cha waimbaji na vyote vya damani sana, anasahau hali yake ya zambi… na sasa wanasema mdanganyifu ni Kacou Filipo. Lakini [ni] mdanganyifu gani, anapo simama mbele ya msichana anamufanyizia yote iliyo mbaya? Hukumuni wenyewe ! Na manabii hao wanasema: « *Tulilipa nafasi hii bei ghali!* » Lakini mulikuwa na haja ya kulipa ile nafasi? Ni ile Yesu alifanya?...

Ikawa na wakati moja ambapo Kweli ilikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Martin Lutheri, tena wakati ambapo ilikuwa ni John Wesley, tena wakati ambapo ilikuwa ni William Branham kama telegram, simu na sasa tuko katikati ya usiku. Angalieni dunia kwa muda mfupi! Katika namna ya kutangaza habari, ilikuwa [kwanza] barua, kisha telegram kisha telefone na sasa ni simu na Internet. Kwa kutembea, ikawa farasi, kisha gari, kisha ndege na sasa ni ndege [inayofika juu ya mwezi] kwa kiwango cha juu sana. Kwa jeshi, ikawa mishale kisha bunduki kisha mabomu na sasa ni silaha za uharibifu na ya bakteriolojia. Hayo yanafwatana na injili nne na pia Ufu.4:7 kwa ukamilifu. Wakati Tunapofikia mwisho, kuna wengine wanao tu ngao, wengine mishale. Imani ni atua kwa atua, nilichapa *" namna ya vibandiko kwa mimea tofauti "* kwa kuonyesha hayo waziwazi.

Ikawa na wakati ambapo simba wa kabila la Yuda, neno, ilitoka pamoja na Paulo kisha ndama ya toleo ilitoka na mamilioni za wakristo wakauwawa kisha, mtu akatoka pamoja na Lutheri, wakati wa uundaji upya. Na tangu nyakati za jioni, tai wanasimama juu ya mafundisho ya uongo na roho za udanganyifu kwani utakaso wa mwili tu hautoshi tena.

Tayari kwa 1817, kampuni ya wachungaji wa Geneva wakakataza kuhubiri juu ya uungu wa Yesu, zambi ya asili, neema na kutangulizwa. Wote waliingia katika maombi na walipata ufunuo inayo pingana, na mutasema kwamba ni Mungu? Mtoto wa Mungu haikumpasa tena kuwa moja wa kampuni hiyo ya kimataifa… munaona? Ni mwanzo wa uharibifu kuu munayo yaona leo.

[…]uongofu wa uchawi katika ukristo ni ya siri mno hata mwanamke mchawi kwa jina la Mamie Sarah anapeleka kujulikana kwake mpaka kuvuka Ghana chini ya kujivika Yesu Kristo. Makanisa katolika, protestanti na za kiinjili, waislamu, wamormoni, wabuda, wabranhamisti,… kila mmoja wa hao anaandika mungu wake na "M" (herufi kubwa)! Ni ukamilifu wa udanganyifu! Yesu Kristo alisema kwamba kama siku hazinge fupishwa, HAKUNA mtu angeliweza kuokolewa.

Nilianza kuhubiri Juma tatu tarehe 08 julai 2002. Nilikuwa nikihubiri katika nafasi ya kungojea gari, vyumba vya wanafunzi wakuu,… Kwa wakati ule, watu walipaza sauti na kusema: "mahubiri nivaquine! Mahubiri nivaquine!…" Ujumbe huu ulikuwa dawa iliyokuja kwa kuwaponya na wakaitupilia. Hata mwanamke mmoja tajiri sana akatafuta kunipatia rushwa ya pesa. Munaona? Ijapo, ninapendelea umaskini kuliko mali ili nifurahie vema kidogo ambacho maskini atanipa. Basi waaminifu kwangu wawe wote matajiri halafu mimi nibaki maskini!

Turudi kwa nukta ya mwanzo, kwa udanganyifu unao tawala ndani ya makanisa na iliyo tu kufunuliwa kwa wana wa ibilisi… Ijapo ukombozi ambao wananenea wote yafwata kanuni. Kwanza inakubidi uwe mkuu na uwe na ile mamlaka. Ni kama polisi wala polisi wa gereza katika vazi ya kazi. Lakini hiyo haitoshi kwani inabidi barua ya amri inayo onyesha siku, saa na pahali. Siyo kwa sababu wewe ni polisi ndipo unaweza kupigia gari filimbi au kufunga mtu. Hiyo ni picha ya mamlaka ya Mungu. Na picha ya mamlaka ya shetani ni jeuri. Anatumia nguvu nje na kinyume ya kanuni iliyo wekwa, pasipo vazi la kazi na ni ile tunaona katika makanisa. Na shetani anajua kwamba hawakupokea hata mamlaka wala amri kwa kumufukuza. Polisi akiwa katika vazi la kazi pamoja na amri, anaweza hata kusimamisha maandamano ya serikali kwa kunyanyua tu mkono wake juu. Munaona? Ile watu wanaita ukombozi ni tu michezo ya shetani mwenyewe. Kwa nafasi ya ukombozi niliona watu wakiamuru mapepo watoke kwa kinywa, kwa uchi, kwa masikio, kwa tundu za pua… na pepo iliwaleta walioshikwa nayo kufanya namna aliambiwa kufanya. Mtu anayefanya hivyo ni musaidizi wa mapepo kama wachawi. Ni wadanganyifu wala siyo kwa Roho ya Mungu wanafanya mambo haya. Niliona utaratibu ya majina za mapepo na watu wanaamini na kufwata mambo yale.

[…] Sifahamu namna gani watu wanaweza kuamini kwamba siku ya kuchukuliwa, kutakuwa na mafurugano ya ndimi za moto za rangi tatu, ndege za kusafirisha zitaanguka kwani wanao endesha watachukuliwa, maredio zitatangaza kupotea kwa watu… NI UWONGO!... ninawaambia kwamba dunia na makanisa hawata tambua HATA KIDOGO. Namna gani katika mateso kamilifu, mkristo anaweza kupatikana kazini hasa kwa uongozi wa ndege? Ninashangaa kusikia uongo huu. Mungu hatasahau wanaotumika kwa ajili ya mambo kama haya, wanapo danganya dunia, kwa mfano wa Yoane Schwab.

Mtu anapokuwa kipofu, anatambua lakini hali ya makanisa ni fumbo. Kuna watu wanao ona ndoto kila mara zaidi ya mbili au tatu kwa usiku moja, ni kazi ya uchawi lakini wanaiweka kwa upande wa Mungu. Ni vigumu kuwakomboa kwani hawawezi kukubali kwamba ni shetani. Wanatamani maombi na baada ya hayo warudi mahali walikuwa. Sala kama hiyo ni ya bure. …Mungu siyo mtu wa makelele. Tangu julai 2002 mpaka leo, kwa miezi nane ya huduma na hata mafungo ya kurejea, kwa yote, sikuona zaidi ya ndoto tano na maono, Mungu ni mshuhuda wangu. Na sija wai kusema: *"Mungu ameniambia"* je! lakini kwa ajili ya hayo mimi si nabii? Ijapo kwa 1995, nilipata zaidi ya ndoto moja karibu kila usiku sawasawa niliieleza katika *"mahubiri juu ya Ufu.14:6-10"*. Manabii wa agano la kale walifanya huduma yao kwa miaka mingi lakini vitabu vya wengi kati yao havifikie ukurasa kumi. Inawezekana hata kwa muda wa miaka tano Mungu hawaambii kitu! Munatambua kwamba wanapotaka kuzungumza, wanasema kwa mfano: *"Kwa mwaka wa tatu ya utawala wa mfalme fulani… Mwaka wa kufa kwa mfalme Ozias… Katika mwaka wa 25 ya kuchukuliwa kwetu, kwa mwanzo wa mwaka..."*. Kwa mara moja tu Israeli alileta hitaji lake kwa Yeremia lakini iliomba siku kumi ili Mungu ajibu. Yer.42 :1-7.

Kwa hayo pia, mutambue kwamba wakati hakuna nabii, Mungu analazimishwa kusema kwa namna ya upekee kwa ndoto, maono na vingine kwa watu wote. Lakini wakati kuna nabii, Mungu anasema kupitia nabii kwa yote inayorudi katika utaratibu wa imani kwa jumla kwa kila ufunuo wa Neno. Munaona? Wakati hakukuwepo nabii, Yosafati akaomba katika 2Sik.20 lakini kulipo kuwa nabii, kwa ile jambo moja tu, mfalme Ezekia alifanya nini? Tusome 2 Wafalme 19: « *na ikafika, mfalme Ezekia alipo sikia mambo haya, akapasua mavazi yake, na akavaa nguo za magunia, na akaingia katika nyumba ya Bwana.* [Kwa kuomba? Hapana! Kwa kuwaalika makuhani waombe? Hapana!] lakni basi akafanya nini? *Akamtuma Eliakimu, aliye wekwa mkuu juu ya nyumba yake, na Shebna, mwandishi, na wazee wa makuhani, wakivikwa nguo za magunia, kwa…* [Kwa nani?] Kwa Isaya, nabii, Mwana wa Amozi; [*Kusanyiko linasema: Amina!]* na wakamwambia nabii: *Ndivyo asema Ezekia: …upandishie basi ombi kwa ajili ya wale ambao wangali wanapatikana».* Mungu akiruhusu nitarudi kwa maelezo haya.

Sisi ni wamoja ya wale ambao tunajua nini tunasema. Munaona? Yesu alisema katika Yoane 4:22: « *ninyi, munaabudu, hamujui nini; sisi, tunajua ambaye tunamwabudu».* Tunarudi katika shauri la Mungu. Kama Musa, Mungu anaweza kunipeleka katika shamba la Edeni kwa kuona ambayo sifahamu ili siku mteolojia mkuu atakapo onyesha ya kutofautiana, nisizubaishwe. Munaona?

Katika 1 Wafalme 22:19-24, nabii Mika alisema: « *niliona Bwana ameketi juu ya kiti chake cha enzi, na majeshi yote ya mbingu wakisimama karibu naye, kuume na kushoto kwake na Bwana akasema: nani ataaminisha Ahaba, apate kupanda na aanguke huko Ramoti-Gileadi? Na huyo akasema hivi, na ule akasema vile. Na roho moja ikatoka na kusimama mbele ya Bwana, na kusema: Mimi nitamwaminisha. Na Bwana akamwambia: namna gani? Na akasema: nitaondoka, na nitakuwa roho ya uongo katika kinywa cha manabii wake wote. Utamwaminisha, na pia utashinda: ondoka, na ufanye hivi. Na sasa, tazama, Bwana ameweka roho ya uongo katika kinywa cha manabii wako wote ambao ni hawa,… Na nabii Zedekia, mwana wa Kenana, akakaribia na kumpiga Mika kwa shavu, na kusema: Roho ya Bwana alipita kwangu na njia gani ili aseme nawe?».* Munaona? Watu hawasomi kwa kujua kwamba Mungu mwenyewe anaweza kutuma roho ya udanganyifu juu ya watu walio wanyofu. Munaona? Haikuwa manabii wa Bali lakini manabii wa Bwana na hesabu yao ni karibu manabii mia nne na hamsini wayahudi na walikuwa wakitabiri kwa moyo wao wote kutoka kwa Mungu lakini Biblia inasema kwamba siku ile walipata kutoka roho mwovu na wao wenyewe hawakujua. Na ni kwa nabii Mika ndipo Mungu alifunulia hayo. Munaona? Mungu ni huru kumfunulia yeyote kama ilivyo mapenzi yake.

Moja ya hatari kubwa ya ukristo, ni hivyo vitabu na barua za maduka hayo yanayoitwa ya kikristo ambavyo juu yake imeongezwa internet wapi watu ambao mwito, wala utume, wala maisha na wanao sukumwa sijui na roho gani, wanaweza kuweka wazi mambo ya kweli. Televisheni ikiwa mbaya, juweni kwamba Internet ni mara kumi mbaya zaidi!... kama kwa watu wanao fwata utaratibu wa uchawi, kila kitabu kinaonyesha kiwango moja na viwango ni mamlaka, mapepo. Mtu kama Osborn, Morris Cerullo, Benny Hinn, Rébecca Brown, Reinhard Bonnke au Yongi Cho anapoandika kitabu moja, mambo anayosema yote inaweza kuwa kweli lakini ni pepo inayojificha nyuma yake. Nyoka, baba yao, aliposema na Eva kwamba wakikula tunda, macho yao yatafunguka na wataweza kujua mema na mabaya kama miungu, ilikuwa kweli lakini nyuma ya kweli hiyo kulikuwa kifo na kuanguka kwa wanadamu. Ni sawasawa. Mambo yote haya ninayo hukumu, mujitenge nayo! Ndivyo asema Bwana, mujitenge na hayo makanisa, munapoalikwa kule, musikwende!

Kumbukumbu la Torati 13:1 inasema nini? Mtu akikuhubiri kweli, na kufanya miujiza, na kutabiri kweli na kisha anakuambia: *"Twende kwa kanisa katolika! Twende kwa kanisa Metodisti! Twende kwa kanisa batisti, pentekoste, foursquare, kusanyiko za miungu, branhamisti,… usikwende! Ni Mungu wako anaye kuweka jaribuni…"* Munafahamu? Biblia haisemi kwamba watafanya yale wanakuwa wakifanya nje ya Mathayo 24:24 na 2 Tes. 2:9-12. Munaona? Ikiwa mtu hana ujumbe utokao kwa Mungu, je! namna gani Mungu anaweza kumupa miujiza na maajabu? Kwa kuthibitisha nini? Kufwatana na Ufu.16:13-14, Biblia inasema kwamba watafanya ambayo wanakuwa wakifanya sasa na wana wa Ibilisi kama Mwanzo 4:17-23 wanatia vitu vyao kwa kazi yao ili waharibu dunia na kutuma nafsi nyingi kuzimu. Munaona kwamba Shetani siyo mjinga? ujumbe wa jioni ulifika kwanza Katadji tangu mwaka 1970 mpaka 72 pale lakini mpaka miaka makumi tatu, sikuona pale kanda wala kusikia jina ya William Branham. Ijapo huko Abidjan, wanajijengea hekalu kubwa kubwa na nzuri sana, wanatoleana ma Mercedes na manyumba za sifa. Na wanapofanya michango, siyo kwa kuhubiri vijiji lakini ni katika lengo la kuunda mikutano kwa kujionyesha na kuvuta wale ambao wameponyoka mazehebu! Oh! Rehema! Wameunda katika Internet nafasi ambapo wameweka ujumbe wa jioni badala ya kutuma wainjilisti duniani. Munaona? Ikiwa Mungu anaweza kukubali hiyo sasa ingemubidi kukubali Daudi wakati huyo alipo tia sanduku ya Mungu juu ya gari mpya. Neno la Mungu bado

halijawai kuchukuliwa na gari mpya na haita chukuliwa hata kidogo na Internet. Internet, ni vizuri lakini inapokamata kabisa nafasi ya wainjilisti, ni hatari.

Ndani ya kusanyiko ambapo nilikuwa nikishiriki, palikuwa na sakafu nzuri sana iliyo pakwa zahabu [*Ndl: mazabahu*] lakini wakaibadilisha! Kuna mwaminifu aliye simama kwa kutoa sakafu ya franga CFA milioni moja. Na kwa meza ya Bwana, mwanamke mmoja alisimama kwa kutoa kikombe cha bei ya franga mia moja au SMIG mara tatu, malipo ya chini ya mfanya kazi wa serkali ya Cote d'Ivoire. Munaona? Ijapo mitume walikunywa katika vikombe vya miti… Ndio maana nilisema kwamba wabranhamisti ni chicha mpya ya uharibifu wa kikristo. Wote pamoja, kwa upande wote, ni wachungaji wa uharibifu.

Sasa Mungu alipo tupatia ufunuo juu ya Biblia, wana wa shetani walisema: *"Tutakwenda kwenyi Internet na huko tutafanya utafiti mkuu juu ya historia na version za Biblia na tutapingana na huyo Kacou Filipo"*. Lakini haizuru nini watakuta kwenyi Internet, haiwezi kunivuruga, ni mtu aliye onyesha maoni yake juu ya jambo fulani. Msimamo wetu siyo Internet lakini Mungu kupitia Nabii mjumbe. [*Kusanyiko linasema "Amina!!!"*]. Zambi yao ya leo ni kama zambi ya Saulo katika 1 Sam.28, wakati Mungu hakumjibu kwa nabii, wala kwa Urimu Tumimu, wala kwa ndoto na maono na hapo akakwenda kuuliza Neno la Mungu kwa mwanamke anaye ita aina yote ya roho. Neno la nabii. Ni wana wa ibilisi, muwaache kimya!... munaamini kwamba Internet ni mwanamke mwenyi kuita aina yote ya roho? [*Kusanyiko linasema: "Amina!!!*].

Na kusema *«Ndivyo asema Bwana »* ambayo wachungaji na manabii wengi wanatumia kwa kuwasemesha manabii wa Biblia ambao tayari wamefariki ni musemwa wa uchawi. Ni roho moja ya uchawi ya Ukatolika, ya desturi za asili, na ya mwanamke mwenyi kuita roho za wafu ambaye Saulo alikwenda kumuona katika 1 Sam.28 na sasa ile roho imejigeuza sura na inatenda kwa namna ya siri katika ukristo. Mungu ni yule yule! Yule yule jana, leo, hata milele! Katika Agano la Kale, katika hali ya baba, alitenda kupitia manabii ambao Neno lililo andikwa ni Ndivyo Asema Bwana hata ikiwa hawasemi « *Ndivyo Asema Bwana »*. Na baada ya kuonekana duniani, alisema ninarudi kwa Baba, katika hali yake ya Agano la Kale pamoja na manabii. Basi roho ya chura na ya uchawi ya ujanja inatoka wapi kwa kusema: « *Ndivyo Biblia inasema »* au « *Ndivyo neno linasema »?* kama Saulo, wanapoona kwamba Mungu hawasemei tena, wanasemesha watu ambao tayari wamekufa. Na mbele ya ushuhuda ya kile ambacho Mungu iko akifanya hapa, wengi kati yao walinikaribia kwa ajili ya maombi na sikose kuwaambia ile ambayo inastahili kuwaambia. Munaona? Inawabidi wafahamu kwamba hawaamini William Branham kuliko mimi; lakinini ninakamata William Branham kama mtu wa Mungu sawasawa na Isaya, Amosi na wengine, wakati yao imepita! Je! Leo kwa mwaka 2006, ukiwa na shida ya kiroho au ya ugonjwa, unaweza kwenda kaburini mwa William Branham kwa kuomba msaada wa maombi? Munatambua kwamba uchawi siyo mbali nanyi? Sijui ukubwa gani alikuwa William Branham na huduma yake lakini Biblia inasema kwamba Mungu wa Biblia siyo Mungu wa wafu lakini Mungu wa waliyo hai. Baada ya Musa mkuu, hata huduma ya nabii fulani iwe ndogo kwa namna munaweza kuiona, ni yeye, ule nabii mdogo, ambaye anashika funguo za ufalme juu ya uso wa dunia na ni yeye inabidi kumusikiliza na kumutangaza.

Vema, tutazame sasa Mwanzo 4:17-24, tuisome: *«* [shairi la 17…] *Na Kaina akajua mke wake, na akachukua mimba na akamzaa Henoka; na akajenga mji, na akaita jina ya mji ule sawasawa na jina la mwana wake Henoka.* [Shairi la 18…] *Na kwa Henoka akazaliwa Iradi ; na Iradi akazaa Mehuyaeli ; na Mehuyaeli akazaa Metusaeli ; na Metusaeli akazaa Lameki.* [Shairi la 19…] *Na Lameki akajitwalia wake wawili: jina la mmoja ilikuwa Ada, na jina la wa pili, Sila.* [Shairi la 20…] *Na Ada akazaa Yabali; yeye, akawa baba ya wenyi kukaa hemani na wanao ufugo.* [Shairi la 21…] *na jina la ndugu yake ilikuwa Yubali: yeye, alikuwa baba ya wote wanao piga kinubi na filimbi.* [Shahiri la 22…] *Na Sila, yeye vilevile akazaa Tubali-Kaina, ambaye alikuwa mfua chuma wa vyombo vyote vya shaba na vya chuma. Na dada ya Tubali-Kaina alikuwa Nama.* [Shairi la 23…] *Na Lameki akawaambia wanawake wake: Ada na Sila, sikieni sauti yangu ; ninyi wanawake wa Lameki, tegeni sikio kwa usemi wangu: nitaua mtu kwa ajili ya kuniumiza, na kijana kwa ajili ya kuumizwa kwangu ;* [shairi la 24…] *kama Kaina atalipiwa kisasi mara saba, Lameki atalipiwa kisasi mara makumi saba na saba. »*

Vema, sasa, musiseme *"Amina!"* ili musiwavute wasiofahamu. Mungu hafanyi jambo ili ionekane nzuri kwa macho na havuti mtu. Vema,… [*Ndl: wakati wa mahubiri, ndugu Filipo anasema kama mtu anaye zungumza na mtu mwingine mbele yake. Pasipo kulalamika, wala kuruka-ruka*]... kwa shairi ya 17, kuna watu wenyi sifa, baba ya warais, mameya, wenyi manyumba kubwa kubwa, wajenzi,… kwa shairi la 19, ni baba ya wanao oa wanawake wengi, wazinifu, watu wa kimapenzi, waundaji wa hoteli, film,… kwa shairi la 20, kuna baba ya wafugaji,… kwa shairi la 21 kuna baba ya wanamuziki, waimbaji, kwaya, waundaji wa muziki,… kwa shairi la 22, kuna baba ya wafumbuaji, wenyi ma sekta, viongozi wa jamii, kampuni za sekta na biashara, kampuni, watu wa kesi,… Munaona? Walipoanza kutia umeme mijini na vijijini, kwa kawaida ilikuwa jambo nzuri lakini zambi ikazidishwa mara saba kwani televisheni, bar, kichaka na sanduku za usiku (boite de nuit) zikafika pamoja. Munaona?... tena pale kwa shairi la 22, tunaona Nama, mwanamke wa kwanza mwenye sifa duniani, mama ya wanawake huru, Yezebeli ni mjukuu wa mjukuu wake. Ni huyu binti ya Kaina aliye fanya onyesho na tangazo ya kwamba mama ndiye mriti wa watoto na ikamleta yeye mwenyewe kushiriki katika uriti wa baba yake ijapokuwa yeye ni mwanamke. Hata watoto wake waliriti kutoka baba yake Lameki. Munaona? Hii uongozi wa mama nyumbani ikaleta zambi kuongezeka kwani wanawake hao walipotazama mali ya wazazi wao, hapo hawajali ndoa na hao ni wanawake wasiyo na haya wala woga, wasiotii na wametayarishwa kwa uhuru wa wanawake. Nama alikuwa na haki ya kuhubiri katika kanisa ya Lameki na leo, ijapo kelele ya katikati ya usiku, wamoja wanaendelea kuimba na kuhubiri katika makanisa za Lameki… Kwa shairi 23-24: ni baba ya wateolojia, shule za mafunzo ya biblia, maprezidenti za makanisa na ya wote wanaotafsiri Neno la Mungu! Mbali mbali na kuweza kuumba kama Mungu, wanatafsiri Neno lake kwa kusema kwamba wao ni sawa na Mungu. Mteolojia wa kweli ni kinywa cha mungu fulani. Munaona? Na ingine yote ni [kutafuta] msaada ya pesa, wadogo na wakubwa, taifa na serkali, wanaweka mamilioni, ndege za anga za kusafirisha, miundo,… kwa ajili ya makanisa na wanamemba wao kwa kudanganya wanao kaa duniani, wale ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo kabla kuweka msingi ya dunia. Kwa sababu, Mungu atakapo inua watoto wake kwa kiwango cha hao, watajiona kama viongozi wa mali ya Mungu ambayo aliwapa kusudi washikilie kazi yake. Na mwana wa Mungu hataweka mali yake kwa kazi ya mchawi, hata ikiwa mchawi huyo anafufua wafu.

Na tunabariki Mungu kwa ajili ya ufunuo wa wana wa shetani. Munaona? Ni kama ndugu zangu binafsi na wale wote wa kijiji changu mahali nilizaliwa na kukomaa; hawaniamini, siyo kwa sababu ya zambi niliyo tenda lakini kwa sababu tulinyonya [maziwa ya] mama moja, tulikuwa mawindoni au kwa uvuvi pamoja,… lakini mbwa mwitu atatoka mbali, watamuamini. Munaona? ile ndio zambi yangu.

Vema,… na leo, tunaona pia kizazi cha hao wana wa ibilisi wakihubiri kwamba mkristo anaweza kufanya siasa, kunywa pombe ya kulevia, kuvuta sigara, kufanya mapenzi mume na mume au muke na muke, kuoa wanawake wengi,… kucheza juu ya mchanga pembeni ya bahari, kucheza mchezo wa kandanda, kutazama mchezo wa kandanda kwenyi televisheni, munaona? Watu hawa walaaniwe! Wandugu kuvaa nguo ndogo ndogo mbele ya wadada, wadada katika nguo za kuvaa wakati wa kuosha mwili. Shetani sasa ni ndani ya kanisa! Kama Paulo ninaweza kupaza sauti: walaaniwe wanao hubiri mambo kama haya! Ikiwa ulikuwa na wake wawili hata tatu unapokujia Neno, inakubidi kuwachunga kama wanawake wako, lakini ukiwa mkristo haupashwe kuwa na wanawake wawili. Munaweza kufanya zowezi, kukimbia lakini mujikinge na kandanda (au mpira), sija cheza bado mchezo wa kandanda au kutazama mchezo wa kandanda au film kwenyi televisheni tangu 1993 nilipopata ono. Na kwa 2002, ninaweza kuhakikisha kwa nguvu yote kwamba ni Roho ya Yesu iliyo nileta kutupa televisheni yangu mpya ambayo nilinunua bei ghali katika duka ya mulebanone kuitupa kwenyi yalala. Tena jana, ndugu moja kutoka ujumbe wa Branham alinionyesha kitabu moja ambapo ndani yake William alisema: *"Hatuna televisheni. Haita patikana nyumbani mwangu, hata kidogo… Mungu aliniambia nisifanye vile "*. Katika ile ile kitabu, anasema: … [*Ndl: Ndugu Filipo anatafuta ukurasa ule*] Haya, tazama ambacho anasema:… Ndiyo, ni pale. Vema, ninasoma: *"sijapata bado mawazo ya kuwa na televishion nyumbani mwangu. Hakika hapana. Sitaki kitu hiki nyumbani mwangu. Ningeiharibu kwa bunduki yangu ya mawindo. Sitaki kuwa na usiano na kitu hiki kibaya. Hakika"*. [Ndl: ni kitabu: *mamlaka ya Mungu kwa kubadilisha* aya.169 na 242]. Sasa, munapotazama filme na michezo ya kandanda namna gani mutafahamu yale Mungu ameleta mbali na televisheni? Munaona? Na kuhusu kandanda, nchi inapo cheza na nchi ingine, ni wale ma Yesu Kristo za makanisa za nchi hiyo wanao pambana na ma Yesu Kristo za makanisa za nchi ingine. [*Kusanyiko linasema: Amina!*]. munaona? Ni mapambano ya mapepo. Tena wale Roho takatifu wao wanawapatia ufunuo ya ushindi. Na kwa kuanza, mapepo za makanisa, mapepo za wapagani na mapepo za waislamu zinapatana katika vita moja. [*Kusanyiko linasema: Amina!!*]. mkristo hana faida katika mambo yale, mujitenge nao!… Munaona?

Na niliona hata wachungaji wa kibranhamisti ambao, wanapotazama mchezo wa kandanda, wakifurahi na kuruka ruka mbele ya vyombo vyao vya televisheni na watu kama hawa watakuja kubishana nami kuhusu Neno? Hapana! Mimi si tayari! Na kuna watu kama hao ambao wamedanganya na kupoteza kabisa nafsi nyingi kwa namna kahaba ana neema mara elfu kuliko wao. Munaona? wanakuwa vizuri duniani lakini kuzimu ina haki juu yao na haichoki kuwahitaji. Munaona? Kama mchungaji au muhubiri hawezi kuja kwa kusema: *"Ndugu, ninaamini ujumbe, na sasa, nifanye nini?"*. Musimushughulikie. Hata Nikodemu mkuu, mkuu wa wayahudi hakuja kumuomba Yesu maelezo. Munaona? Kilindi inaita kilindi. Na ninapoona kwamba mtu ananiswali kwa kupingana na ujumbe, ninamupa majibu yatakayo musukuma asiamini tena. Jana kuna mmoja aliye nikumbusha kwamba kuna nyongezo katika kitabu kufwatana na maandiko ya mwanzo na kwamba si vizuri. Munaona? Ningeweza kumupa Yer.36:32 lakini nilimuhakikishia kwamba ana sheria. Lipondo! [*Ndl: Kusanyiko inacheka*]. Je! Mimi ni Mungu kwa kuaminisha mtu? Munaona? Ambacho nilipokea toka kwa Mungu na ni kile nimesema, na Mungu alijua kwamba nitaisema hivi! Wakati yangu, ni kwa wale ambao tayari wameamini! [*Ndl: Kusanyiko linasema: Amina! Ndugu Filipo anacheka*].

Vema …kama Biblia inavyosema, Mungu analeta nabii wakati taifa lake limepotea kabisa na anakuja kuleta tena Kweli na kurudisha watu kwa nuru. Ndio maana kabla Malaika na Mwana Kondoo washuke, kulikuwa na patwa mwezi (jua). Na kabla ya haya, unabii za Biblia tayari zilionyesha kwamba kwa wakati fulani, kwa nafasi fulani, Mungu atafanya jambo fulani. Haikubidi kwenda kufunga chakula muda wa siku 21 au 40 na kuja na upako. Yote munayoita *"mafungo Esitheri"*, *"mafungo Yosafati"* wala ingine, ni kujitesa, na hiyo ni Shetani! Na watu wanafwata nyuma ya hayo pasipo kujua kwamba ni zile zile roho za uchawi ndio zinakuwa pale. Ikiwa hamuoni katika Osborn na wengine picha ya wachawi kwa hiyo hamuja zaliwa upya. Lakini wachaguliwa wanao heshima kwa Biblia na Neno la unabii wanakuwa sasa katika kiwango ingine, mbali na uchawi kufwatana na Ufu.12:14.

[…] na ninafikiria kwamba Mungu akisimamisha mtu leo, anapaswa kushinda magonjwa yote ya wakati yake. Kwa wakati wa jioni ilikuwa saratani na katikati ya usiku ni ukimwi. Siku moja tutakapo unganisha ujumbe huu katika kitabu moja, tutafanya kitabu cha ushuhuda na ninasema kwamba kutakuwa na ushuhuda ya uponyaji wa ukimwi, inayohakikishwa na waganga kama sivyo mimi ni nabii ya uongo. Hakuta kuweko mapepo kwa kuleta hiyo kushindwa. [*Kusanyiko linasema «Amina! »*]. Ikiwa Mungu wa kelele ya katikati ya usiku siye Muumbaji wa mbingu na dunia, na kama mimi si Mat.25:6, nisiponye ukimwi. Ile munayoona ni ndogo karibu na ile inayokuja! Yesu Kristo, Malaika wa tarehe 24 aprili 1993 ataifanya. [*Kusanyiko linasema "Amina!"*]. Basi Mungu awape wana wa Ismaeli hao wabranhamisti walio fukuzwa toka wepo wake mali [nyingi] ya vitu na kwetu sisi, atupatie uwezo kwani inabidi wafu wafufuliwe tena, inabidi vipofu waone, inabidi viziwi wasikie,…kwa sababu inabidi Mungu athibitishe Neno na ni kule tunaelekea sasa. Na nimesema kwamba ukimwi haita shinda. Nitaomba hasa mtihani (test), na tena watu watakwenda kufanya uchunguzi upya na tutaichunga pamoja na maelezo ya waganga kwa ushuhuda. Niliona hiyo hatua juu ya makutano waliokuja kwangu. Itakuwa hatua ingine ya huduma yangu na ni lazima ifike. Wakati waliyo tayarishwa kupokea pasipo alama watakapo kataa, inabidi basi mawe zipaze sauti kwa furaha. Mukiona katika Biblia, inakuwa hivi kila mara. Asante Mungu!

Hakuna awezaye kuamini ujumbe huu pasipo kupatwa na matokeo juu ya maisha yake ya kiroho, ya kimwili na ya kijamii. [*Kusanyiko linasema "Amina!"*]. Yote inafwatana na ginsi unaikamata! Muiamini neno moja kwa moja, pasipo mawazo na ninawachokoza ili mutaniambia kwamba yeye si yule yule jana, leo hata milele… Ombi langu ni kwamba Mungu athibitishe kila mara neno hili na ataifanya. Na tunangojea kila mara tafsiri ya njiwa wawili ambayo itabadilisha hakika mwendo wa mambo. Nina uhakika kamilifu baada ya miezi nyingi ya huduma kwamba watu wa makanisa haya wanajua sasa kwamba wao ni juu ya njia mbaya lakini namna gani watarekebisha desturi ambayo walikuta? Na ikiwa wataifanya, watapoteza msimamo

wao ya uchungaji na sasa namna gani watashughulikia jamaa yao, kulipa nyumba zao? Kuna kile wanafikiria na kile wanafanya. Ndio maana Bwana hakuchoka kusema *"wafarisayo na wasadukayo wanafiki!"* wanafanya bidii yao yote kuonyesha waamini picha ingine ya ukweli! Munaona?

Mwana wa shetani ambaye amejazwa teolojia akija kukuambia: *"Huyu Kacou Filipo ni mdanganyifu, anataka kupeleka watu wote kwake ijapo ambayo Mungu anatuomba, ni kuchunguza kile ambacho Yesu alisema na hiyo, unaweza kuifanya pahali pote, katika haizuru sunagogi gani, ukiwa mubatisti, metodisti, kusanyiko la miungu, adventisti au sijui nini. Utofauti ya mafundisho si kitu!!! Ni kama watu weusi, wa kimanjano na wazungu. Mbinguni kutakuwa watu wa aina moja!!! Sisi ni bustani ya Mungu iliyo na mauwa mbalimbali!!! Aleluya!…"*. Akisema hivi nawe unakaa pale kumusikiliza kama Eva, shauri lako. Lakini asubuhi hii, hata kama mimi ni adui yako kama siku ile, nilipokuwa nikihubiri hazarani, mtu yule alitaka kuni… watu walimuzuia lakini hakupenda. Alisema: "mimi ni tayari kuchukua zambi ya Kaina". Munaona?… lakini hata hivi, kwa neema niliyopewa, ninawaambia kwamba, haizuru miujiza ngapi mulipata mikononi mwa watu hawa, musiwaache tena kuwawekea ninyi mikono. Na ninyi waafrika, ikiwa baada ya kupokea mema mengi kutoka wachawi wa asili, leo munasema kwamba ni shetani inayo tumia watu hawa, namna gani hamufahamu yale niko nikiwaambia?

Kuna kanisa moja tu na wanaingia ndani yake kwa Neno. Mungu atakapo tuma mtu kama mtumishi, mtu huyu atakuja pamoja na Neno, ujumbe ya wakati yake. Hataunda kanisa lakini kuja na Neno kwani katika mwanzo haikuwa kanisa lakini Neno na ni kwa nguvu ya Neno ndipo kanisa inaundwa. Watu wanakusanyika kando ya ile ujumbe na ile inaitwa Kanisa.

Mungu aamshe mbegu yake ndani mwetu na atie kiu ya Neno lake mioyoni mwetu! Mungu afanye viriba vyetu vya zamani tupu na atupatie Roho Mtakatifu. Mungu ajifunue kwa watoto wake na akusanye wachaguliwa wote wa pande nne za dunia kando ya Habari Njema iliyo ahidiwa tangu zamani za kale na ambayo sasa imefunuliwa mbele yetu. Kwa sababu heshima, hekima, baraka, shukurani na utukufu na uwezo kwa kuifanya ni kwake! Amina!

Ijapo, munyanganyi mmoja alinaswa akitengeneza kartasi za benki. Wasitaki wake wakamupeleka kwenyi polisi na kusema: *"Tulikamata mtu huyu akitengeneza kartasi za benki na tazama mfano moja…"*. Polisi akatwaa ile pesa, akaichunguza na kusema: *"Mabwana, pesa hii ni ya kweli!"*. Wakajibu tena na kutia mkazo: *"Lakini bwana polisi, ni yeye aliye tengeneza hii kartasi!"* polisi akamgeukia munyanganyi na kusema: *"Bwana ni wewe uliyetengeneza hii pesa?"*. Akajibu *"Ndio!"*. Na polisi akaongeza kusema: *"Ijapokuwa anakubali, hatuwezi kumuhukumu kwani pesa hii ni ya kweli!"*. Na munyanganyi akawekwa huru. Munaona? Mbele ya watu, munayofanya ni haki, sawa, na kamilifu, lakini kuna moja ambaye, siku moja, atawahukumu… aliye na masikio ya kusikia asikie!

[*Ndugu moja anasema kwa lugha*...]

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org